

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



Tarehe: 20 Mei, 2019

**TANGAZO LA ZABUNI - LINARUDIWA**

**ZABUNI Na. LGA/020/2018--2019/NCS/13 – 14**

**ZABUNI YA KUPATA WAKANDARASI WENYE MAGARI NA MITAMBO YA KUFANYA USAFI, KUZOA TAKA NA KUZISAFIRISHA KWENDA DAMPO LA CHIDAYA NA, KUKUSANYA ADA YA USAFI KUTOKA KATIKA MAKAZI, BIASHARA NA TAASISI MBALIMBALI KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.**

1. Halmashauri ya Jiji la Dodoma inakusudia kupata wakandarasi wenye magari na mitambo ya kufanya usafi, kuzoa taka na kuzisafirisha kwenda dampo la Chidaya na, kukusanya ada ya usafi kutoka katika 1akazi, biashara na taasisi mbalimbali katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa kipindi cha kuanzia **Julai, 2019** hadi **June, 2021**.
2. Halmashauri ya Jiji ya Dodoma inapenda kuwaalika wakandarasi wenye magari na mitambo ya kufanya usafi, kuzoa taka na kuzisafirisha kwenda dampo la Chidaya na, kukusanya ada ya usafi kutoka katika 1akazi, biashara na taasisi mbalimbali katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutuma maombi yao kwa zabuni zifuatazo:-

<b>Na.</b>	<b>ENEO LA USAFI</b>	<b>NAMBA YA ZABUNI</b>
1.	Eneo hili linahusu kata ya Nkuhungu	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/13</b>
2.	Eneo hili linajumuisha kata za Ipagala, na Dodoma Makulu	<b>LGA/020/2018-2019/NCS/14</b>

3. Zabuni hii itaendeshwa katika taratibu za mfumo wa Ushindani wa Kitaifa (National Competitive Bidding) kama ilivyoelekezwa katika Kanununi za Ununuzi zilizotolewa kwa tangazo la serikali namba 446 la mwaka 2013 na

marekebisho yake ya mwaka 2016 isipokuwa itakapokuwa imeandikwa vinginevyo kwenye masharti maalum ya uombaji (Bid Data Sheet).

4. Wenye nia ya kuomba zabuni hii wanaweza kupata taarifa za ziada na kukagua nyaraka za zabuni katika ofisi ya Katibu – Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Jiji la Dodoma Mkao Makuu, gholofa ya kwanza, chumba namba 14, S. L. P. 1249, Dodoma, kuanzia saa 1.30 asubuhi hadi saa 9.30 mchana, Jumatatu hadi Ijumaa isipokuwa siku za mapumziko ya ki-Taifa.
5. Wenye nia ya kuomba zabuni hii wanatapata **Nyaraka za Zabuni** katika lugha ya Kiswahili baada ya kulipa ada ya **Shs. 100,000/= (shilingi laki moja tu)** ambayo haitarejeshwa (**non - refundable**). Malipo hayo yalipwe kwa **Mkurugenzi wa Jiji, Jiji la Dodoma, S. L. P. 1249, Dodoma.**
6. Mwisho wa kupokea zabuni ni tarehe **03/06/2019** saa nne (4) asubuhi, na ufunguzi utafanyika mara baada ya muda wa mwisho wa kupokea zabuni hizo mbele ya waombaji watakao amua kuhudhuria kwenye ukumbi ya mikutano ulioko jengo la Makao Makuu ya Jiji (zamani likijulikana kama jengo la CDA), ghorofa ya pili.
7. Zabuni zote zitumwe zikiwa zimefungwa ndani ya bahasha iliyofungwa ipasavyo. Juu ya bahasha ioneshwe namba ya zabuni. Zabuni zitumwe kwa anuani ifuatayo:-  
**Mkurugenzi wa Jiji,  
Jiji la Dodoma,  
S.L.P 1249,  
DODOMA.**
8. Zabuni ambazo zitachelewa kwa muda uliopangwa na zabuni zitakazotumwa kwa barua barua pepe (e-mail) hazitapokelewa.

Bartazar Ngowi,  
**Kaimu Mkurugenzi wa Jiji  
JIJI LA DODOMA.**